**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI**
**(EWURA)**

**NAMBA YA MALALAMIKO: GA.71/135/LZ/2024/32**
**NAMBA YA LOIS: COMP-2024-00000272**

**KATI YA**

**JOHN RAPHAEL MASUBI ..........................................................................MLALAMIKAJI**

**NA**

**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA ................................................ MLALAMIKIWA**

---

**AMRI**

---

***(Imetolewa na Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA tarehe 12 mwezi Februari 2025)***

**MALALAMIKO HAYA** yameletwa mbele ya Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kwa ajili ya kutoa uamuzi leo tarehe 12 mwezi Februari 2025, kwa madai kwamba Mlalamikiwa abadilishe nguzo iliyooza iliyosimikwa karibu na nyumba ya Mlalamikaji mtaa wa Greenview-Lumala, Kata ya Kiseke, Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza.

Baada ya kupokea malalamiko tarehe 10 Disemba 2024, Mamlaka (EWURA) ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi wake kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kanuni ya 6 (1) na 7 (1) ya Kanuni

za EWURA za Utatuzi wa Migogoro - (*EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure), Rules 2020*)).

Mnamo tarehe 27 Januari 2025, Mlalamikiwa aliwasilisha utetezi wake na kukiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kuifahamisha Mamlaka kwamba amekwisha badilisha nguzo hiyo na kuvuta nyaya ambazo zilikuwa zimekaribia kugusa ardhi. Vilevile, Mlalamikiwa ameomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza. Baada ya kupokea utetezi kutoka kwa Mlalamikiwa, Mamlaka iliwasiliana na Mlalamikaji ili kutaka kufahamu kama ni kweli Mlalamikiwa ameshayafanyia kazi malalamiko yake kama alivyodai kwenye utetezi wake. Mlalamikaji alituma ujumbe kwa Afisa wa Mamlaka kupitia simu namba 0677 022776 akithibitisha kwamba malalamiko yake yamefanyiwa kazi na Mlalamikiwa. Hivyo basi, Mlalamikaji anaomba kuondoa shauri lake EWURA.

Katibu wa Bodi **ANATOA AMRI** kwamba malalamiko haya yanaondolewa na kila upande utabeba gharama za uendeshaji wa malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) hapa Dodoma leo tarehe 12 mwezi Februari 2025.

..............................

**TONI S. MBILINYI**
**KATIBU WA BODI**